**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**689** **VITENDO VYA KUJIFUNZA SAYANSI**

**Muda: Saa 3.** **Mwaka : 2007**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C.**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka katika kila sehemu **B** and **C**.
3. Sehemu **A** ina alama **40** na sehemu **B** na **C** zina alama 30 kila moja.
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. (a) Taja stadi mbili (2) za msingi za utambuzi ambazo hutumiwa katika majaribio ya kisayansi.

   (b) Orodhesha hatua tatu (3) za msingi katika kuandika ripoti ya jaribio.

2. (a) Nini maana ya neno "dhana tete" katika utafiti wa kisayansi?

   (b) Taja vifaa vitatu (3) rahisi vinavyoweza kutumiwa kufanya jaribio la kunyonya maji darasani.

3. (a) Bainisha faida tatu (3) za kufuata utaratibu maalumu katika kufanya jaribio.

   (b) Eleza kwa kifupi umuhimu wa kuchora matokeo ya majaribio.

4. (a) Orodhesha kanuni nne (4) za usalama lazima kuzingatiwa wakati wa majaribio ya moto.

   (b) Eleza njia mbili (2) za kuwatambulisha wanafunzi wa elimu ya awali dhana ya "kuelea na kuzama".

5. (a) Fafanua **aina nne (4)** za uchunguzi zinazoweza kufanywa na mtoto.

6. Ainisha **kanuni nne (4)** za kutunza vifaa vya maabara/majaribio darasani.

7. (a) Taja faida tatu (3) za kufanya makundi ya wanafunzi wakati wa majaribio.

   (b) Eleza kwa kifupi changamoto mbili (2) za kufundisha Hisabati kwa vitendo.

8. (a) Bainisha tendo moja (1) la kujifunza ambalo linaonyesha uhusiano kati ya Sayansi na lugha.

   (b) Eleza sifa tatu (3) za mwalimu bora wa Vitendo vya Kujifunza Sayansi.

9. (a) Orodhesha **njia nne (4)** zinazoweza kutumiwa kurekodi matokeo ya uchunguzi.

10. (a) Eleza kwa kifupi faida mbili (2) za kutumia vifaa vya asili katika majaribio ya sayansi.

    (b) Taja mambo mawili (2) yanayoonesha umuhimu wa utafiti wa utendaji kwa mwalimu.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU B (Alama 30)**

Jibu maswali mawili (2) kutoka katika sehemu hii.

11. (a) Jadili mambo sita (6) ya kuzingatia ili kuhakikisha usalama wa mtoto wakati wa kufanya jaribio la kutumia umeme mdogo.

    (b) Fafanua faida nne (4) za kuruhusu watoto kuuliza maswali wakati wa majaribio.

12. (a) Eleza hatua tano (5) za kuwafundisha wanafunzi wa elimu ya awali stadi ya "kulinganisha na kutoa tofauti" kwa kutumia mifano halisi.

    (b) Bainisha mambo matano (5) yanayoonesha umuhimu wa stadi za kusoma katika Vitendo vya Kujifunza Sayansi.

13. (a) Kwa nini majaribio ya vitendo ni muhimu katika kufundisha sayansi kwa watoto wadogo? Toa sababu tano (5).

    (b) Eleza maana na umuhimu wa mafunzo yakiendelezo (mafunzo kazini) kwa walimu wa somo la Vitendo vya Kujifunza Sayansi.

**SEHEMU C (Alama 30)**

Jibu maswali mawili (2) kutoka katika sehemu hii.

14. Jadili namna mwalimu wa somo la Vitendo vya Kujifunza Sayansi atakavyofundisha dhana ya "sumaku na uvutano" kwa kutumia njia zifuatazo:

(a) Njia ya Maonyesho.

(b) Njia ya Mchezo wa Kuigiza.

15. (a) Fafanua maana ya ufundishaji unaozingatia ujuzi na faida tatu (3) zake.

    (b) Tofautisha upimaji wa awali na upimaji tamati. Eleza jinsi kila moja inavyotumika katika somo hili.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

16. (a) Jadili nyanja zote tatu (3) za upimaji wa kielimu: Utambuzi, Hisia, na Utendaji kwa kutoa mfano mmoja (1) kwa kila moja.

(b) Bainisha changamoto tano (5) zinazokabili utekelezaji wa mtaala wa Vitendo vya Kujifunza Sayansi nchini Tanzania.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org